



Baba yetu uliye Mbinguni,  
Kwa Roho wako tunaunganishwa ki-imani, matumaini na upendo. Pamoja  
na kujitenga na kuwa wapweke wakati huu, tu watoto na jumuiya yako ya  
kiulimwengu.

Kuza imani zetu kwa sababu kila wakati uko karibu nasi, tuunganishe na  
kaka na dada zetu ulimwenguni.

Wainue wagonjwa. Imulike miyo ya wapweke. Wape hekima na nguvu  
wanaokabiliwa na majukumu.

Waimarishe watenda kazi mahospitalini.

Uwe na ndugu zetu wote ulimwenguni.

Na utupe mawazo mapya yatakayoimarisha umoja wetu.

Bwana akubariki na kukulinda;

Bwana akuangazie Nuru ya uso wake na kukufadhili;

Bwana akuinulie uso wake na kukupa amani.

Amina

#### KWA PAMOJA-

*Maombi kiulimwengu. Kama unataka kuwa mshiriki katika maombi hata  
ya mnyororo. Shiriki sala hii kwenye makundi yako mitandao ya kijamii,  
au chapa (printi) na weka sala hii mlangoni, au ukutani au dirishani au  
kwenye gari lako. Tumetengwa kimwili lakini Kiroho tuko pamoja-  
Tuoneshe hili!*

(Translation: Anderson Moses Kipande)